## Vitate

Hebu tazama maneno yafuatayo na kwa kifupi ueleze yana sifa gani
Baba papa
Ngoa ng'oa
Faa vaa
Doa ndoa
Paka baka
Kupwa kubwa
Make the highlighted letters blink
Provide space for typing in the correct answer

**Jibu**
Maneno haya yanakaribiana kimatamshi japo maana ni tofauti.
Andika maana zaidi ya moja ya maneno yafuatayo:-
Barabara
Ila
Provide space for learner to type in
Majibu
Barabara – Njia kuu
-Sawasawa / shwari / sawa
2. Ila - kasoro / dosari
Zoezi 4
Kamilisha methali zifuatazo
Baada ya dhiki

Mti mkuu ukigwa

Mjinga akierevuka

Kinyozi

Riziki kama ajali

Simba mwenda pole

**Faraja**

Wana wa ndege huyumba / huwa mashakani
Mwerevu yuko mashakani
Hajinyoi
Huitambui ijapo / ikija
Ndiye mla nyama

sauti, silabi na maneno
Sauti ndicho kipashio au kipengele cha chini kabisa katika lugha. Sauti hutumiwa kuunda silabi za maneno. Kwa mfano;

Maneno baba,oa na mjomba yameundwa kwa sauti zifuatazo:-
Baba ; b+a+b+a
Oa; o+a
Mjomba; m+j+o+m+b+a

Kabla ya kujenga maneno, sauti hizi hujenga silabi. Silabi ni tamko moja katika neno k.m.
; Ba+ba ; = baba
; O+a; = oa
; M+jo+mba;= mjomba
; Ndwe+le; = ndwele

Kama inavyodhihirika katika mifano hii, silabi inaweza kujengwa na:-Konsonati + irabi b+a
Irabi peke yake / o/a
Konsonati peke yake m
Konsonati mbili +irabi a'mb+a
Konsonati tatu + irabi a' ndw+e

**Zoezi 3**
Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiambishi sahihi cha upatanisho wa kisarufi.
Ulinzi mkali __tahitajika wakati wa maonyesho ya ukulima.
Marashi hayo __nanukia vizuri.
Sukari __liyopo __nawatosha nyote.
Kucheza kwa vijana wetu __liwavutia watu wengi.
Pale ndipo _lipomwagwa takataka.
Kule __nakolimwa __nahitaji kupandwa mbegu za mchicha.
Mle __nakohamia __nataka kutakaswa.

Majibu:-
Ulinzi mkali utahitajika wakati wa maonyesho ya ukulima.
Marashi hayo yananukia vizuri.
Sukari iliyopo inawatosha nyote.
Kucheza kwa vijana wetu kuliwavutia watu wengi.
Mahali ambapo panapolimwa panahitaji kupandwa mbegu ya mchicha. .
Mahali ambako kunalimwa kunahitaji kupandwa mbegu za mchicha.
Mahali ambamo mnalimwa mnahitaji kupandwa mbegu za mchicha.
Ugali __napendwa na wakenya wengi.

**Zoezi**

Andika kulingana na maagizo yaliyo kwenye mabano
Nyumba iliyojengwa imebomoka (katika hali ya ukubwa)
Mito ile imefurika (hali ya udogo)
Kikoba kile kilichopotea kimepatikana (hali ya kawaida)
Kidole kilicho umia kimetibiwa (hali ya ukubwa)
Maduka ya rejareja yaliyofunguliwa yana bidhaa nyingi (hali ya udogo)

KIDATO CHA KWANZA

Kiguo kilichoraruka kimeshonwa (hali ya kawaida)

Jumba lililojengwa limebomoka
Vijito vile vimefurika
Mkoba ule uliopotea umepatikana
Dole lililoumia limetibiwa
Viduka vya rejareja vilivofunguliwa vina bidhaa nyingi
Nguo iliyoraruka imeshonwa
Ngeli ya KI-V

Ngeli hii hujumuisha nomino za vitu visivyo na uhai ambazo huchukua kiambishi ki cha upatanisho wa kisarufi katika umoja na vi katika wingi .Kwa mfano
Cheti kilikabidhiwa aliyefuzu

Vyeti vilikabidhiwa waliofuzu
Kijia kile kinaelekea mtoni

Vijia vile vinaelekea mitoni

Kitambulisho kilichopatikana barabarani ni cha Wafula
Vitambulisho vilivyopatikana barabarani ni vya akina Wafula.

**Zoezi**

Chagua kiambishi mwafaka ili kujaza pengo:-
Serikali itakabiliana vilivyo na ugonjwa ___naoua mifugo (a, i, u)
Serikali zitakabiliana vilivyo na magonjwa ___nayoua mifugo.(zi, ya, i)
Nyumba (umoja) ___kijengwa vizuri haibomoki. (a, i, zi)
Nyumba (wingi) ___kijengwa vizuri hazibomoki (zi, wa, ya)
Ulimi ___nawatia wengi matatani (i, u, zi)
Ndimi ___nawatia wengi matatani (zi, ya, i)
zi

**NGELI YA U-U;**

Ngeli hii hujumuisha nomino zinazorejelea vitu visivyoweza kuhesabika kama vile wema, ujinga, uji, udongo. Kwa kuwa vitu hivi haviwezi kuhesabika, kiambishi cha upatanisho wa kisarufi huwa U. Mfano
Unga wa mchicha nafaka unatumika kupikia vyakula vingi kama ugali, chapatti, uji, mchuzi.
(Provide an animation/picture of a packet of amaranthus flour with ugali,cuisine, uji, chapatti in a kitchen environment)
Mchanga shambani umezombwa na mafuriko (Provide an animation/picture of flood water causing soil erosion)
Uzembe darasani utakufanya uporomoke.( Provide an animation/picture of a class with some students sleeping as the teacher is teaching)
Utangulizi

KIDATO CHA KWANZA

Onyesha viambishi tamati katika vitenzi vifuatavyo kwa kutumia mkwaju.
Walikubaliana
kilisomwa
Zimekataliwa
Tumeimbisha
Highlight the following parts as the answers
– a/na
– wa
– li/wa
– i/sha
Kauli za kunyambua Kuendelea
f. Kutendea, hali hii huonyesha kupokea tendo

nguo zimeanikwa
k.m. Mti umepand/wa/
Nyama imechom/wa/
Mto umevuk/wa/
Shamba litalim/wa/
Vitenzi katika kauli hii huisha na na – wa, lewa au liwa
g. Kutendesha; - Katika hali hii mtu au kitu fulani husababisha mtu / kitu
Kingine kutenda jambo fulani
Pia hutumiwa kuonyesha hali ya kulazimisha
k.m. Kuendesha, rusha, pikisha, zamisha
Vitenzi katika kauli ya kutendesha huisha –ish, -esh, z, na, lish

**Maudhui**
Katika baadhi ya mashairi ujumbe, maudhui au habari wa mtunzi hujitokeza wazi lakini katika mashairi mengine ujumbe umejificha. Kwa mfano shairi hili ujumbe umejitokeza waziwazi kama vile watoto kuajiriwa, kunyimwa haki zao na kunyanyaswa.

**Kazi ya ziada**

Tafuta tahadhari zingine tano ambazo hukujifundisha katika somo hili na uambatanishe na michoro yake na zingine ambazo haziambatani na michoro
Provide a printable worksheet for the student to DRAW.jpg.
Uandishi wa Ratiba
Umewahi kualikwa kwenye sherehe ya arusi?
Unakumbuka msururu wa yaliyotendeka?
Pasi kuwa na ratiba, ingekuwa vigumu watu
kuelekezwa na matukio kupangika hadi ikawa
harusi ya kufana. Kabla ya siku yako ya
sherehe, shuhudia inavyoandikwa ratiba.
Kielelezo cha Ratiba
Ifuatayo ni ratiba ya arusi;
Ratiba ya Arusi baina ya Bi. Hidaya na Bw. Fikirini:

Siku: Jumamosi
Tarehe: 27 Nov 2009

**Mahali pa sherehe:**
Kanisa la mtakatifu Francis wa Assisi, Mlaleoni
Ukumbi wa Rahatele, Mlaleoni
8.30 – 9.30 asubuhi: Bi Arusi achukuliwa nyumbani kwa wazazi wake
9.30 – 10.00 asubuhi: Safari kuelekea kanisani
10.00 – 10.30 asubuhi: Kufika kanisani na kujiandaa kwa ibaada
10.30 – 12.00 mchana: Ibaada ya Arusi
12.00 – 12.30 mchana: Kupiga picha
12.30 – 1.30 Mchana: kuelekea kwenye ukumbi.

1. – 2.30 alasiri: Mlo na vinywaji
2. – 3.30 alasiri: Mawaidha:

Mwakilishi wa wazazi wa kuumeni
Mwakilishi wa wazazi wa kuukeni
Mwakilishi wa kanisa
Mwanakijiji
3.30 – 4.30 jioni: Kutoa zawadi
4.30 – 5.00 jioni: Kukata keki
5.00 – 5.15 jioni: Kutoa shukrani
5.15 jioni: Maombi ya kufunga sherehe na watu kufumukana
Ngeli ya Ya-YA
Ya-Ya; Ngeli hii hujumuisha nomino zinazorejelea vitu au matendo ambayo hayabainiki kama yako katika hali ya umoja au wingi na ambazo huchukua kiambishi Ya cha upatanisho wa kisarufi. Mfano;
Maziwa yanahitaji kuchemshwa vizuri.

Mali yake yote yanatoka shambani mwake.

Mafuta ya petroli yamepanda bei maradufu.

Ngeli ya I-I
I-I; Ngeli hii hujumuisha nomino ambazo hazihesabiki na zinazochukua kiambishi I cha upatanisho wa kisarufi. Mfano;
Theluji katika mlima Kenya inayeyuka kwa kasi sana.

Chumvi inatia ladha katika chakula.

Kenya imetia sahihi mkataba wa maelewano ya kimaendeleo na Uchina.

## Ngeli ya KU

Ku; Ngeli hii hujumuisha nomino zinazotokana na vitenzi. Aghalabu nomino hizi hurejelewa kama nomino-kitenzi na huchukuwa kiambishi ku cha upatanisho wa kisarufi. Mfano;
Kukwea ukuta kwake kuliwashangaza wengi. (Provide an animation/picture of a girl scaling a wall at a supersonic speed and many spectators getting astonished)
Kuvuta sigara kwao kumewaletea magonjwa;

**Ngeli ya Mahali**

Ngeli ya mahali. Ngeli hii hugawika mara tatu kulingana na viambishi awali vya upatanishowa kisarufi. Navyo ni;
Pa/po. Hiki huonyesha mahali mahsusi panapojulikana au panapoonekana. Mfano.
Pale barabarani pamemwagika petroli.

Hapo mlipoketi pana siafu.

Ku/ko Hiki huonyesha mahali kusiko dhahiri au kusikojulikana vizuri. Mfano.
Huku kuna starehe na anasa nyingi

Huko kwao kuna maendeleo mengi.

Mu/mo Hiki huonyesha mahali ndani ya kitu. Mfano.
Mle ukumbini mumejaa watu.

Shimoni mlimoingia panya mna nyoka.

Ngeli katika hali ya Udogo na ukubwa
Nomino katika hali ya udogo huingia katika ngeli ya KI-VI
nazo nomino katika hali ya ukubwa huwa katika ngeli ya LI-YA
kwa mfano;

**Ngeli ya U-YA**

Ngeli hii hujumuisha nomino zinazorejelea mambo tusiyoweza kuyaona lakini tunaona matokeo ya mambo haya. Nomino hizi ni kama vile ugonjwa, ubaya, ukubwa nk ambazo huchukua kiambishi cha upatanisho U katika umoja na Ya katika wingi. Km.
Ulezi umekuwa mgumu sana siku hizi.

Malezi yamekuwa magumu sana siku hizi. (Provide an animation of parents on the dining tables in deep thought of what to provide to malnourished their children with tattered clothes and empty utensils)
Ugonjwa aliougua umemmaliza si haba.
(Provide an animation/picture of an emaciated person unable to walk due to effects of a disease)
magonjwa waliougua yamewamaliza si haba. (Provide an animation/pictture of emaciated people unable to walk due to effects of diseases)
(Provide blinking hazards for the highlighted syllables)

**Ngeli ya U-ZI**

KIDATO CHA KWANZA

Ngeli hii hujumuisha kundi la nomino ambazo huchukua kiambishi cha upatanisho U katika umoja na Zi katika wingi. Kwa mfano:
Ukuta umekamilika kujengwa.

Kuta zimekamilka kujengwa.

Uzi unafuma sweta.

Nyuzi zinafuma sweta.
Uta ulitumika katika mashindano ya kulenga shabaha ya wanajeshi.

Nyuta zilitumika katika mashindano ya kulenga shabaha ya wanajeshi.

MAZUNGUMZO KULINGANA NA MUKTADHA
Lugha utakayoitumia shuleni ni tofauti sana na utakayoitumia hotelini na hata unapozungumza na marafiki wakati wa likizo. Ukweli ni kwamba matumizi ya lugha hutegemea muktadha. Somo hili litakusaidia kuainisha miktadha tofauti na lugha inavyotumika humo.
Zoezi la 1
Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kujaza viambishi awali vinavyofaa
Mwanafunzi ___lipongezwa ___lipofaulu katika mahojiano na wazazi wake
Wanafunzi ___lipongezwa ___lipofaulu katika mahojiano na wazazi wao.
Kifurushi ___lichoibwa ___mepatikana
Vifurushi ___livyoibiwa ___mepatikana
Msitu ___nafaa ___hifadhiwa
Jino ___lilooza ___mengolewa
Meno ___liyozaa ___mengolewa
Majibu:
a, a
wa, wa
ki,ki
vi,vi
u,u
i,i
li, li
ya, ya
Provide positive reinforcement for the correct answer using ‘vyema’.
Provide encouraging reinforcement for wrong answer using ‘jaribu tena’.
Give the learner a chance of 2 trials before providing the correct answer.

**USHAIRI**

Akili By Mathias Mnyampala
Mpima jambo la mbele, huyo anayo akili,

KIDATO CHA KWANZA

Mpima hili na lile, hakosi mtu adili,

Hasa mtu kama yule, sifa anastahili,

Mtu hapati akili, ila mpima ya mbele.

Ili kufanikisha sherehe kama hizo ni lazima kuwe na mpango maalumu ambao utafuatwa ndipo sherehe ziendeshwe vizuri. Mpango huu huitwa RATIBA. Yaani utaratibu unaoonyesha matukio yanayotarajiwa kutendeka (hatua kwa hatua) Hatua hizi hujikita kwa muda uliowekwa. Shughuli fulani huchukua muda mahususi ambao huandikwa kwenye ratiba. Kwa kifupi, ratiba huonyesha jambo litakalofanywa, nani atakayehusika na wakati wa kutekeleza.
Ifuatayo ni ratiba ya arusi;
Tarehe: 27 Nov 2009

Mahali pa sherehe: Kanisa la mtakatifu Francis wa Assisi, Mlaleoni
8.30 – 9.30 asubuhi: Bi Arusi achukuliwa nyumbani kwa wazazi wake
9.30 – 10.00 asubuhi: Safari kuelekea kanisani
10.00 – 10.30 asubuhi: Kufika kanisani na kujiandaa kwa ibaada
12.30 – 1.30 Mchana: kuelekea kwenye ukumbi.

1. – 2.30 alasiri: Mlo na vinywaji
2. – 3.30 alasiri: Mawaidha:
3. – 4.30 jioni: Kutoa zawadi
4. – 5.00 jioni: Kukata keki
5. – 5.15 jioni: Kutoa shukrani
6. jioni: Maombi ya kufunga sherehe na watu kufumukana

Mambo yanayozingatiwa katika uandishi wa Ratiba
Katika uandishi wa insha ya ratiba mambo yanayozingatiwa ni;-
Kichwa cha ratiba
Mahali pa sherehe
Tarehe
Mwili wa ratiba
Upande wa kushoto huandikwa saa ya kufanyika kwa tukio nao upande wa kulia tukio lenyewe linafuata hadi mwisho wa ratiba kulingana na matukio yalivyopangwa.
Ikumbukwe kuwa, uandishi wa ratiba hutegemea aina ya sherehe na muda uliotengwa. Muda hurejelewa kwa kuzingatia utaratibu wa usomaji saa wa kimataifa.
Zoezi
Hebu tazama picha zifuatazo kisha uzipange ukizingatia utaratibu wa matukio katika sherehe hii.
Present a mix up of a prize-giving ceremony in this order
Hotuba ya mgeni wa heshima
Maombi ya kufunga mkutano
Wanafunzi kuketi ukumbini
Matumbuizo
Maombi ya kufungua sherehe

Wazazi kufika
Hotuba ya mwenyekiti, halmashauri ya shule
Kutuzwa kwa zawadi
Hotuba ya mwenykiti, jumuiya ya wazazi na walimu
Kutoa shukrani
Hotuba ya mwalimu mkuu
3. Wanafunzi kuketi ukumbini
6. Wazazi kufika
5. Maombi ya kufungua sherehe
4. Matumbuizo
11. Hotuba ya mwalimu mkuu
9. Hotuba ya mwenyekiti, jumuiya ya wazazi na walimu
7. Hotuba ya mwenyekiti, halmashauri ya shule
1. Hotuba ya mgeni wa heshima
8. Kutuzwa kwa zawadi
10. Kutoa shukrani
2. Maombi ya kufunga mkutano
Provide reinforcement as 'hongera' for correct order of events and 'jaribu tena' for incorrect order.
This should be organized in such a way that from the first event and every subsequent event there is a response.
Allow two trials.

**Shughuli**

Katika sehemu hii, utapata maelezo zaidi juu ya somo husika. Bonyeza mada yoyote kati ya zilizoorodheshwa ili ufaidi!

Matumizi ya lugha katika muktadha
Mojawapo ya sifa zinazotawala matumizi ya lugha katika jamii ni muktadha
lugha inatumika,wahusika na uhusiano wao pamoja na lengo la mawasiliano.
Katika sehemu hii unatakiwa kubonyeza mazoezi yaliyoorodheshwa ili uweze kujipima iwapo umeyapata yaliyofunzwa katika somo hili. Vilevile unaweza kuupima uelewaji wako wa mada hata kabla hujashughulikia mafunzo ili uweze kujua unayopaswa kutilia mkazo zaidi.

**Matumizi ya Lugha Shuleni**

Hebu tuone vile muktadha wa shuleni unavyotawala matumizi ya lugha.Tazama na usikilize video ya mazungumzo kati ya mwalimu wa zamu na wanafunzi shuleni.Zingatia matumizi ya lugha katika muktadha huu halafu ujibu maswali yanayofuata.

**Hitimisho**

Imedhihirika ya kwamba lugha katika muktadha fulani hutawaliwa na lengo linalotokana na haja au shughuli inayoendeshwa katika muktadha huo,wahusika,uhusiano kati yao na umri wao.
Matumizi ya Lugha Mtaani
Tazama na usikilize video ya mazungumzo kati ya vijana mtaani.
Chunguza matumizi ya lugha katika muktadha huu halafu ujibu maswali yanayofuata

**2. Ila - kasoro / dosari**

- isipokuwa

Provide positive reinforcement for correct answers 'vizuri sana' and encouragement for incorrect answers 'jaribu tena'.
Allow learner to try twice then give correct answer

**Shadda**

Maana mbalimbali za maneno 'barabara' na 'ila' zinatokana na kile tunachokiita shadda. Shadda ni mkazo unaowekwa kwenye silabi fulani za neno wakati wa kutamka ili kutoa maana inayolengwa na mzungumzaji.Mathalani,tulipoweka mkazo silabi ya pili ya neno bara'bara,tulipata maana yake ni sawasawa, shwari au sawa.
Tunapotamka neno lilo hilo, yaani 'barabara' bila kuweka mkazo wowote, maana yake inabadilika na kuwa njia kuu au baraste. Kama tulivyofanya katika neno barabara,tunaweza kuweka mkazo tunapotamka neno ila na kupata maana mbili tofauti.
Tunatambua kuwa tukiweka shadda baada ya silabi ya kwanza kama vile i'la, maana inayolengwa ni dosari au kasoro au udhaifu.Hata hivyo,tukitamka neno lilo hilo bila kuweka mkazo wowote,maana inakuwa Isipokuwa au lakini.
Tanbihi
Ikumbukwe kuwa shadda na kiimbo hutawaliwa zaidi na alama hisi (!), kiulizi (?)na kikomo / kitone (.) katika maandishi.Bila shaka,tumetambua kuwa sentensi tuliyotamka ni ile ile. Hata hivyo, sentensi hiyo hiyo inaweza kutamkwa kwa namna mbalimbali na kuwasilisha ujumbe tofauti.Tunapoongea, sauti huweza kupanda na kushuka kutegemea lengo la mawasiliano. Kupanda na kushuka kwa sauti husababisha kuwepo kwa mkazo ambao hudhihirisha maana inayodhamiriwa na mzungumzaji.
Mathalani, huenda msemaji angetaka:Kuarifu au kutoa kauli ya taarifa Kwa mfano, Nilifunguliwa lango.
Kuamrisha;Kwa mfano, Fungua lango!
Kutoa rai au ombi. Kwa mfano, Nifungulie lango.
Kuuliza Kwa mfano; Nifungue lango?
Kuonyesha hisia kama vile kushangaa, kubeza au kudharau.
Kwa mfano; Umefungua lango!

1. Kuarifu au kutoa kauli ya taarifa:Kwa mfano, Nilifunguliwa lango.
2. Kuamrisha; Kwa mfano, Fungua lango!
3. Kutoa rai au ombi. Kwa mfano, Nifungulie lango.
4. Kuuliza Kwa mfano;Nifungue lango?

5.Kuonyesha hisia kama vile kushangaa, kubeza au kudharau.; Kwa mfano; Umefungua lango!

## Maana ya Kiimbo

**Maana ya Kiimbo**

Ukirejelea sentensi ya Anakula nyoka maana tatu zinajitokeza kutegemea kupanda na kushuka kwa sauti (kiimbo) wakati wa kuzungumza kwa mfano.

Anakula nyoka. Hii ni kauli ya taarifa. Mtu anafahamishwa ujumbe.

Anakula nyoka!- Hii yaonyesha hisia labda za kushangaa. Mtu anashangaa kwa kusikia ujumbe huo na anarudia kwa njia inayoonyesha hisia za kushangaa.

Anakula nyoka? -Hii ina maana kuwa swali limeulizwa. Yawezekana mtu ameona kana kwamba mwingine anakula hicho kinacholiwa, lakini hana uhakika na ndipo anauliza ili apate uhakika.

**Umuhimu wa Shadda na Kiimbo**

Tumeweza kutambua kuwa shadda hutokeza kwenye silabi katika neno tunapotamka.
Kiimbo nacho hutokeza katika sentensi tunapozungumza.Hizi ndizo tofauti za kipekee kati ya Shadda na Kiimbo.
Shadda na kiimbo ni hali mbili za kimatamshi ambazo ni muhimu sana katika mazungumzo.Kutokana na shadda, maana inayodhamiriwa katika neno hujitokeza.Vivyo hivyo, ni kutokana na kiimbo ndipo tunaweza kubainisha anacholenga kuwasilisha mzungumzaji katika sentensi.

Vitate na Vitanza Ndimi

Umemudu? Jiburudishe na uboreshe matamshi yako.
vitate

**Maana ya Vitate**
Maneno yanayokaribiana kimatamshi lakini maana zake ni tofauti kama tulivyoona hapo awali huitwa VITATE.
Kwa mfano
Zana ;sana,
Tosha ; tosa/toza.
Vitanza Ndimi

Hebu; Sikiliza vitanza ndimi vifuatavyo vikitamkwa kisha uvitamke kwa usahihi na kwa muda uliopewa.
Viatu vile vitatu ni vya watu watatu waliotatua hali tata kwetu Jumatatu. (Tamka kwa sekunde 5)
Mamluki amerukia milki ya malkia na mali ya Miriamu. (Tamka kwa sekunde 5)
Wanawali wa Awali hawali wali wa awali ila wali wao.(Tamka kwa sekunde 5)
Ali hali kwa kila hali maana hana hali. (Tamka kwa sekunde 3)
Matata yenye utata unaotatiza ya dadake Tata yalitatuliwa na dadake Tatu. (Tamka kwa sekunde 5)
Maana ya Vitanza Ndimi
Bila shaka, umekabiliana na changamoto katika kutamka sentensi ulizopewa hasa kwa muda uliotolewa. Sentensi hizi ni mifano ya vitanza ndimi.

Hili ni fungu la maneno yanayotatanisha wakati wa kuyatamka kwa sababu ya kuwepo kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi. Aghalabu watu wengi hukwama wanapojaribu kutamka vitanza ndimi na wengine hushindwa kuvitamka.

KIDATO CHA KWANZA

1.Hebu; Sikiliza vitanza ndimi vifuatavyo vikitamkwa kisha uvitamke kwa usahihi na kwa muda uliopewa.

Provide the following in sound. Get a person who can pronounce the given Kiswahili tongue twisters correctly and within the shortest time possible.

Viatu vile vitatu ni vya watu watatu waliotatua hali tata kwetu Jumatatu (Tamka kwa sekunde 5)
Mamluki amerukia milki ya malkia na mali ya Miriamu (Tamka kwa sekunde 5)
Wanawali wa Awali hawali wali wa awali ila wali wao(Tamka kwa sekunde 5)
Ali hali kwa kila hali maana hana hali (Tamka kwa sekunde 3)
Matata yenye utata unaotatitiza ya dadake Tata yalitatuliwa na dadake Tatu (Tamka kwa sekunde 5)
2. Hebu Vitamke vitanza ndimi vifuatavyo kwa usahihi na kwa muda uliopewa.
(Let the learners pronounce the tongue twisters within the given time. Then provide the right pronounciation in sound by getting a person who can pronounce the given Kiswahili tongue twisters correctly and within the shortest time possible. The learner can gauge their pronounciation)
Kadogo mdogo alifinyanga udongo wa kutengeneza vyungu vidogo (Tamka kwa sekunde 3)
Kuku wako na vikuku vyako haviko huko kwake viko kwako (Tamka kwa sekunde 3)
Lori lile la Lari lenye rangi limeregea rege rege. (Tamka kwa sekunde 3)
Mto ule umefura furifuri na kuwafurusha watu wenye safura. (Tamka kwa sekunde 4)

Hebu Vitamke vitanza ndimi vifuatavyo kwa usahihi na kwa muda uliopewa.
Kadogo mdogo alifinyanga udongo wa kutengeneza vyungu vidogo. (Tamka kwa sekunde 3)
Kuku wako na vikuku vyako haviko huko kwake viko kwako. (Tamka kwa sekunde 3)
Umuhimu wa Vitanza Ndimi
Vitanza ndimi vina umuhimu mkubwa hasa katika jamii kama ifuatavyo;
Huwafunza na kuwazoesha wanajamii kuwa na matamshi bora na hivyo kuimarisha matamshi.
Hujenga uwezo na ukakamavu wa kuongea au kuzungumza bila kutatizika.
Hufikirisha hasa ndipo mtu aelewe maana ya anachokisema.
Hukuza uwezo wa ubunifu.
Hunoa bongo za wanajamii ambao baadaye wanaweza kuwa walumbi.
Huburudisha wanajamii.
Hujenga stadi ya umakinifu katika kusikiliza.

**Maana ya Methali**
Methali ni semi fupi za kimapokeo zinazotueleza kwa muhtasari fikira au mawazo mazito yanayotokana na uzoefu na tajriba ya jamii .
Methali huwasilisha ujumbe wake kwa matumizi ya lugha ya mafumbo na inayojenga picha akilini mwa mwanadamu.

Zoezi 1
Onyesha kipande cha kwanza na kipande cha pili katika methali zifuatazo kwa kutumia alama ya mkwaju
Vita havina macho
Chovya chovya humaliza buyu la asali
Kuteleza si kuanguka
Chururu si ndo ndo ndo
Ngoja ngoja huumiza matumbo
Mwenye macho haambiwa tazama

KIDATO CHA KWANZA

Vita / havina macho
Chovya chovya / humaliza buyu la asali
Kuteleza / si kuanguka
Chururu / si ndo ndo ndo
Ngoja ngoja / huumiza matumbo
Mwenye macho / haambiwa tazama
The blue stroke indicates the division required. Provide positive reinforcement for correct answers ‘vyema / vizuri’ and an encouragement for wrong answers ‘jaribu tena’
Sifa za Methali
Methali ni mojawapo ya vipera vya semi katika fasihi simulizi
Methali huwa na sifa zifuatazo;-

1. Huwa maneno machache yanayoweza kukumbukwa kwa urahisi. Kwa mfano: heshima si utumwa,Mwerevu hajinyoi
2. Mara nyingi huwa na vipande viwili kwa mfano,

Kipande cha kwanza................ Kipande cha pili
Mwangaza mbili.........................Moja humponyoka
Asiyekubali kushindwa................ Si mshindani
Mchumia juani............................ Hulia kivulini
3. Sifa nyingine ya methali ni kuwa hutumia picha au istiari. Istiari ni ulinganishi uliofichika ambapo maneno ya kulinganisha kama vile mithili ya, mfano wa na kadhalika hayatumiki.
Hebu tazama picha zifuatazo

Mpanda ngazi hushuka
Mtaka cha mvunguni sharti ainame
Ujana ni moshi ukienda haurudi
Dalili ya mvua ni mawingu
Kila ndege huruka kwa bawa zake

5. Methali nyingi hujengwa kwa kutia chuku au kutia chumvi.Kwa mfano
Polepole ya kobe humfikisha mbali
Ulimi ni upanga
Mfinyanzi hulia gaeni
Maji ya kifuu bahari ya chungu

6. Aghalabu kipande cha kwanza kinaweza kikapingana na kipande cha pili. Kwa mfano:-
Kipande cha kwanza.............................Kipande cha pili
Haraka haraka ............................ haina baraka
Amani haiji ................................ ila kwa ncha ya upanga
Mtaka yote ................................ hukosa yote
Mwenye shibe ............................ hamjui mwenye njaa
Kulenga.................................... si kufuma

**Umuhimu wa methali**

Mbali na sifa zake methali pia zina umuhimu wake katika jamii. Kwa mfano:-
1. Kueleza na kutahadharisha jamii kwa mfano,Asiyeskia la mkuu huvunjika guu
2. Kuadilisha jamii kwa mfano, Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
3.Kufahamisha juu ya utamaduni, historia na mazingira ya watu, kwa mfano, Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
4.Kupevusha akili, kwa mfano,Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe

**Sauti,Silabi na Maneno**

Kabla ya kujenga maneno,sauti hizi hujenga silabi. Silabi ni tamko moja katika neno. kwa mfano,
Ba+ba ; = baba, O+a; = oa, M+jo+mba;= mjomba
Ndwe+le; = ndwele
Konsonati mbili +irabi mb+a
Konsonati tatu + irabi ndwe+le

**Sentensi**

Hebu tazama jinsi maneno tuliyojenga yanaweza kuunda sentensi.
Sentensi ni mpangilio wa neno au maneno kisarufi unaoleta maana.
Kuna aina tatu za sentensi.
Hizi ni Sentensi sahili, ambatano na changamano.
Sentensi Sahili huwa ni sentensi iliyojengwa kwa kitenzi kimoja.
kwa mfano
Mwanafunzi anasoma.
Mjomba amevaa kanzu.
Sentensi ambatano huwa ni sentensi mbili sahili au zaidi zilizounganishwa kwa kutumia kiunganishi, kwa mfano,
Dobi alifua nguo kisha akazipiga pasi.
Ekomwa amechaguliwa kama diwani na kisha akateuliwa kuwa meya.

Sentensi changamano huwa ni sentensi iliyoundwa na sentensi mbili sahili ambazo zinategemeana.sentensi moja sahili haiwezi ikawasilisha maana bila sentensi sahili ya pili.
kwa mfano,
Yiene aliyepita mtihani wake vizuri amepata mfadhili.
Watoto wanaorandaranda mtaani watasakwa na kupelekwa shuleni
Mifano ya sentensi,

1. Wazazi hawashindwi kuwalea watoto
2. Kila mtu anapenda kuwa bingwa
3. Unafaa kuwa kimya katika maktaba
4. Vijana wanacheza mpira

**Nomino na Vitenzi**
Maneno yanayotumiwa kutajia vitu, viumbe, mahali, au hali kama tulivyoyaona huitwa NOMINO.
Vile vile kuna maneno ambayo hutumiwa kurejelea vitendo katika sentensi. Maneno haya huitwa VITENZI. Kwa mfano,Kimbia

sukumana
Panda
Nawa

**Mizizi na Viambishi katika Vitenzi**
Hebu tazama vitenzi vifuatavyo;-
ana/pik/a
ata/pik/a
wata/pik/a
ameni/pik/ia

ana/imb/a
tuli/imb/iwa
mna/imb/iana
uli/imb/wa

Sehemu iliyo katika kisanduku huitwa mzizi wa kitenzi. Hii ni kwa sababu haibadiliki kitenzi kinaporefushwa mwanzo na mwisho wa mzizi.
Sehemu zinazotanguliza mzizi huitwa kiambishi awali[ana/pik/a], na zinazotokea baada ya mzizi huitwa kiambishi tamati [ana/pik/a] .

Vivumishi
Pia kuna maneno ambayo hutumiwa kueleza zaidi kuhusu nomino. Maneno haya yenye kutoa sifa huitwa vivumishi kwa mfano;

Gari nyekundu
Nyumba kubwa
Mzee kipara
Nyumba mbili

Kuna aina nyingine za maneno ambayo hutumika katika sentensi.Aina hizi ni;-
Viwakilishi ni maneno au viambishi vinavyosimama badala ya nomino kwa mfano,

1. Lendeni alikuja.Tunaweza dondosha nomino Lendeni na tukasema Alikuja.Hapa kiambishi a kinasimama badala ya nomino Lendeni
2. Maduka yote yalifungwa. hapa tunaweza dondosha nomino maduka na tukasema yote yalifungwa. yote ni kiwakilishi kinachosimama badala ya nomino maduka.
3. Wakulima walipata hasara mwaka jana.Wao walipata hasara mwaka jana.katika sentensi ya pili wao ni kiwakilishi kinachosimama badala ya nomino wakulima
4. Mambo unayoambiwa unafaa uyazingatie kwa makini.

Hayo unayoambiwa yafaa uyazingatie kwa makini. Hayo ni kiwakilishi kinachosimama badala ya nomino mambo.
Vielezi;ni maneno ambayo hufahamisha zaidi kuhusu kitendo.Yanajibu maswali kama vile kitendo kilitendeka wapi?vipi?namna gani?lini? na kilitendwa mara ngapi?

1. Baba aliamrisha kijeshi. Neno kijeshi ni kielezi.
2. Tulikimbia uwanjani mara nyingi. Neno mara nyingi ni kielezi.

Viunganishi ni maneno yanayotumika kuunganisha maneno mengine, vifungu au sentensi.

1. Chagua kitabu cha hisibati au cha sayansi. Neno au ni mfano wa kiunganishi.
2. Walifika vijana kwa wazee.

Vihisishi ni maneno yanayoonyesha hisia mbalimbali kama vile hofu,furaha, mshangao, wasiwasi na kadhalika.

1. La Hasha!sitakubali kashfa hiyo.
2. Salale!Mtoto huyo amenusurika ajali hiyo.

Vihusishi ni maneno yanayotumiwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya vitu viwili au zaidi.

1. Vitabu viko juu ya meza
2. Tangu mwakilishi wetu achaguliwe haonekani kijijini.

## Ngeli

Kwa mujibu wa upatanisho wa kisarufi, Kiswahili kina ngeli zifuatazo :-

Ngeli ya A-WA
Ngeli ya KI-VI
Ngeli ya U-I
Ngeli ya LI- YA
Ngeli ya I-ZI
Ngeli ya U-U
Ngeli ya Mahali PA-KU-MU,
Zoezi la 1

Ngeli hii hugawika mara tatu kulingana na viambishi awali vya upatanisho wa kisarufi.
Navyo ni;Pa/po. Hiki huonyesha mahali mahsusi panapojulikana au panapoonekana.
Mfano.
Pale barabarani pamemwagika petroli.

Ku/ko Hiki huonyesha mahali kusiko dhahiri au kusikojulikana vizuri.

Mu/mo Hiki huonyesha mahali ndani ya kitu.
Mle ukumbini mmejaa watu.

Nomino katika hali ya Udogo na ukubwa
Nomino katika hali ya udogo huingia katika ngeli ya KI-VI nazo nomino katika hali ya ukubwa huwa katika ngeli ya LI-YA

Ni muhimu kukumbuka kuwa:-

Nomino zote za viumbe wenye uhai ziko katika ngeli ya A-WA
Nomino zote katika ngeli ya KU huundwa kutokana na vitenzi
Ngeli ya YA-YA huusisha nomino ambazo kwa kawaida huwa majina ya vitu majimaji.
ANDIKA KULINGANA NA MAAGIZO YALIYO KWENYE MABANO :-
Kijia kile kinaelekea mtoni
Mnyambuliko wa Vitenzi

**Maana ya Mnyambuliko**
Mnyambuliko ni hali ya kuvuta kitenzi kwa kukipa viambishi tamati ili kuleta maana nyingine

Sehemu zilizo katika kisanduku zinaonyesha mnyambuliko katika kauli mbalimbali kama ifuatavyo
Sentensi zufuatazo zinahusu kitenzi katika kauli ya kutenda katika hali zilizotajwa.
Bainisha hali hizo na sentensi hizi

**Kauli za kunyambua**
Tenda - hii ni hali ya kufanya kitendo kwa mfano, cheka, imba, ruka ,safiri

**Tendewa -** mtu hutendewa kitu / jambo na mwingine.
Pia mtu / watu hutenda jambo kwa niaba ya mwingine / wengine

kwa mfano, Alichekwa, somewa, imbiwa, rukiwa, safirishwa.
Vitenzi katika kauli hii huishia na -iwa, -ewa, -liwa, lewa

**Tendeka: -** Huonyesha kutendeka au kukamilika kwa jambo fulani. Wakati na mtendaji havitiliwi maanani.
kwa mfano, Chekeza, imbika, rukika, safirika.Vitenzi katika kauli hii huishia na -ika, -ka

**Tendeana**: - Hii ni hali ya pande mbili kutendeana, upande mmoja unatenda na ule mwingine unatenda vile vile.Vitenzi katika hali hii huishia kwa -ana

**Kutendea: -** Kitenzi katika kauli hii hudokeza yafuatayo;
Kifaa fulani kilitumiwa kutekeleza kitendo Fulani
Kitendo kilitendewa mahali fulani
Sababu ya kitendo fulani
Kitendo kuelekea mtu au kitu fulani
Kitendo kilitendwa kwa niaba ya mtu fulani
Vitenzi katika hali ya kutendea huisha na -ia au -ea

**Kauli za kunyambua ii**
Kutendea, hali hii huonyesha kupokea tendo

mfano,
Mti umepand/wa/
Vitenzi katika kauli hii huisha na - wa,- lewa au -liwa

**Kutendesha; -** Katika hali hii mtu au kitu fulani husababisha mtu / kitu
Kingine kutenda jambo fulani
Pia hutumiwa kuonyesha hali ya kulazimisha
kwa mfano, Kuendesha, rusha, pikisha, zamisha

KIDATO CHA KWANZA

Vitenzi katika kauli ya kutendesha huisha -ish, -esh, - za, na,-lish

Nukta mkato/ semi koloni hutumiwa kutenganisha sentensi iliyo ndefu sana. Kwa mfano:(1) Hakuna jambo rahisi maishani; kijana, ukitaka cha mvunguni lazima ujitolee na ustahamili kuinama.(2) Mto wa Nairobi umechafuliwa sana; Itabidi tuungane mikono kuusafisha na kuhakikisha kuwa maji yake ni safi na yanaweza kutumiwa na binadamu pamoja na wanyama.

1.Nukta pacha /koloni hutumika kutanguliza maneno yaliyo katika orodha.Mfano:Mama alienda sokoni akanunua matunda: maembe, mapera, mafenesi,parachichi, matikiti, mapapai na machungwa2.Kuonyesha maneno ya msemaji katika mtindo wa tamthilia kwa mfano:Cherop: Njagi yuko wapi?Kariuki: AmetokaCherop: Na Simiyu atakuja leo?Kariuki: Bila shaka.3. Kutenganisha saa na dakika au saa,dakika na sekunde.Mfano10:30, 11:25:32 4.Katika misahafu kama vile Korani na Bibilia kuonyesha sura na aya.Luka 3:7-12Yunus a.s, 4:163

**Parandesi/mabano hutumiwa:**

Kubainisha sauti za lugha mfano[a], [e], [i ], [o], [u ]
Kufungia nambari au herufi katika kuorodhesha. Mfano, kuwasili kula kulala na kadhalika
Hutoa maelezo kwa waigizaji kwa mfano, Achieng (akilia) Kwa nini unaniacha? (anasinasina)Hutumiwa kutoa ufafanuzi zaidikwa mfano,Mombasa (mji wa pwani ya Kenya) ni maarufu sana kwa Utalii.Hubana kisawe cha maneno au kufungia maneno yanayotangulia au maelezo kuhusu neno katika sentensikwa mfano Ami ( nduguye baba) amefika.
Alama hisi hutumiwa kuonyesha hisia za moyoni kama vile furaha, mshangao,uchungu,mshtuko,majuto, huzuni na kadhalika, Mfano:

1. Lo!mtoto amevunja sahani!
2. Hongera!
3. Umefuzu mtoto mzuri !
4. Laiti ningalijua! Nisingelimkopesha!
5. Pole! Sikujua ulipata msiba.

Kuna alama nyingine zaidi za kuwakifisha kama vile:
ritifaa ( ' )
kiulizi (?),
mkwaju/mshazari (/)
alama za mtajo/za kunukuu/za usemi ('')
herufi kubwa (H, E)
Kufikia mwisho wa somo hili uweze
Kutaja na kueleza baadhi ya sheria katika mashairi ya arudhi.
Kueleza ujumbe wa mtunzi wa shairi.
Maana ya Shairi
Kutokana na zoezi ulilofanya umeona kuwa shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu kwa lugha ya mkato.
Asili ya shairi ni nyimbo.
Zamani watu walikuwa wakiimba nyimbo za:-

kuwabembeleza watoto walale
jandoni
harusi
Nyimbo hizo zikaja kuwekwa kanuni za utunzi kama vile vina, mizani, beti na kisha ushairi ukatokea.

**Zoezi1**
Sema kweli au si kweli.

Umuhimu wa shairi

Kufundisha maadili mema kama vile heshima, usafi, ukarimu, kusaidiana na kuvumiliana
Kuikosoa jamii na kuipa mwelekeo kama vile kurekebisha maovu kama ufisadi, kujaribu kuishauri jamii kuhusu jinsi ya kukabiliana na magonjwa kama vile ukimwi na njaa
Kuburudisha.

**Mateso ya Watoto**

1.Ninalia na kulia, nakumbuka na umia,
Namwomba naye Jalia, nipate cha kutumia,
Nikikumbuka dunia, nataka hata zimia,
Mateso yetu watoto, ni Mola anayejua.

**2. Ofisa kanichukua, kule kwetu ni Bungoma**

Nikaletwa Kaliua, nikamlelee Wema
Maendeleo amua, miezi sita kukwama,

**3.Baba kuwa safarini,nanyimwa nacho chakula,**

Malalo yangu bandani,kunukiwa na milala,
Mapema osha sahani,na mabaki ninakula.
Mateso yetu watoto,ni Mola anayejua.

**4.Mwili wangu,kidhofika,babu auliza hali,**
Nami kujibu nataka, mama kazidi ukali,
Wapi nitenda fika, ndugu kwa Mola wasili,

**5. Nilikwenda migodini, napo kumbukumbu kovu,**
La kufikiwa shimoni, mguu wangu mbovu,
Sasa nami masikini, nimebaki mlemavu,

**Katika shairi ulilosoma umetambua ya kwamba:-**

Lina beti tano- ubeti ni kifungu kimoja au mgawanyiko maalum unaopatikana katika shairi
Vina (kwa umoja Kina) ni sauti zinazotokea katika mwisho wa kipande cha mshororo.
Mizani ni silabi au tamko moja katika neno la shairi
mshororo ni msitari mmoja katika shairi

kibwagizo ni mshororo unaorudiwa katika beti

**Maana na umuhimu wa kamusi**

Kamusi ni kitabu kinachohifadhi maneno yanayopatikana katika lugha fulani katika kipindi fulani cha wakati. Kamusi ni muhimu sana kwa jamii:
Hutoa maelezo ya maana za maneno na kutupa ufafanuzi unaotusaidia kuelewa maana za maneno mapya au mazito tunayokumbana nayo katika lugha.
Hutuwezesha kufahamu namna maneno yanavyoendelezwa
Hutuangazia aina ya neno yaani kama neno ni nomino, kitenzi, kiwakilishi, kivumishi, kielezi, kihisishi au kihusishi
Hutuelekeza namna ya kutumia neno fulani. Aghalabu kamusi nyingine zinapotoa maelezo ya neno hufuatiliza na kuonyesha jinsi neno linavyotumiwa katika sentensi

Hutudokezea visawe vya maneno
Hutuonyesha kama neno hubadilisha umbo lake katika wingi toka umoja
Hufahamisha namna kitenzi kinavyoweza kunyambuliwa

**Mpangilio wa maneno**
Kamusi huyapanga maneno kwa njia ambayo humrahisishia mtumiaji kuyarejelea kama ifuatavyo:
Maneno hupangwa kwa utaratibu wa kiabjadi au kialfabeti kuanzia A - Z kwa mfano

Amana
Amani
Bakuli
Baraza
Baridi
Chai
Chura
Daima
Dira
Wehu
Yai
Zama

Ikiwa sauti za kwanza katika maneno zinafanana kwa mfano kama katika maneno Amana na Amani, mtu huenda kwa sauti ya pili, ikiwa pia hizo zinafanana, huenda kwa ya tatu au ya nne kama hali hiyo inajitokeza kwa sauti ya tatu, huendelea na hali hii mpaka sauti zitakapotofautiana, hapo ndipo huangalia ile inayokuja kwanza kiabjadi.
Maneno hupangwa kwa njia elekezi. Pale juu pembeni mwa ukurasa huwekwa neno linalotangulia kutolewa maelezo katka ukurasa huo.Haya humrahisishia mtumiaji kukadiria kwa wepesi pale atalipata neno analolitafutia maana na hivyo kuokoa wakati.
Iwapo neno ni kitenzi, kiambishi 'ku' kinachotangulia vitenzi hudondoshwa. Hivyo:
Kuchota huwa Chota
Kufariji huwa Fariji

Kupamba huwa pamba
Kusafiri huwa Safiri
Kutembea huwa Tembea

**Matumizi ya Vifupisho**

Kamusi hutumia vifupisho kuonyesha aina za maneno ya Kiswahili,mathalani;
(N) - Nomino
(T) -Kitenzi
(V)- Kivumishi
(W) -Kiwakilishi
(E) -Kielezi
(U) -Kiunganishi
(I) -Kihisishi

Hali kadhalika, kunavyo vifupisho vya maneno mbali mbali vinavyotumika katika kamusi navyo ni kama vile;

Taz ikimaanisha; tazama
M.f ikimaanisha; mfano
K.v ikimaanisha kama vile
N.k ikimaanisha; na kadhalika
M.t ikimaanisha; methali
Ms ikimaanisha; msemo
Nh ikimaanisha; nahau

## Umoja na Wingi

**Kamusi pia hutambulisha umoja na wingi wa nomino.**

Kitenge (N) vi -(vi-ni kiambishi kinachoonyesha wingi wa kitenge yaani vitenge)
Binadamu (N) (Hii haikuwekewa kiambishi chochote kwani hubakia vivyo hivyo katika umoja na wingi)
Shamba (N) ma ;(ma-ni kiambishi kinachoonyeshawingi wa shamba yaani mashamba)
Mgomba (N) mi - (mi -ni kiambishi kinachoonyesha wingi wa mgomba yaani migomba)

**Kufikia mwisho wa somo hili uweze:-**

Kujeleza maana ya tahadhari
Kutaja na kueleza sifa za matumizi ya lugha katika tahadhari
Kufasiri ujumbe katika picha na alama za tahadhari
Kueleza umuhimu wa tahadhari

**Maana na matumizi ya Tahadhari**

Zoezi ambalo tumekamilisha hapo awali linahusiana na alama za tahadhari.Tahadhari ni ujumbe unaotoa ilani au onyo kwa watu ili kuwatanabahisha kuhusu jambo fulani.Jambo tunalotanabahishwa nalo huenda

likawa la hatari au jambo ambalo mtu hafai kulifanya kwani linaweza kuwa na madhara fulani. Aghalabu ujumbe katika tahadhari hutolewa kupitia kwa maneno yaliyoteuliwa kwa uangalifu na kuwekwa kwa muhtasari. Aidha,ujumbe huu hupitishwa pia kwa njia ya michoro, picha, alama au ishara. Kwa mfano;

Tahadhari hizi zinatolewa kwa njia ya michoro au ishara.Tahadhari zinazotolewa kwa njia hii huweza kufupisha ujumbe mrefu ambao ungehitaji kuelezwa kwa maneno mengi. Hata hivyo, michoro na ishara hizi huhitaji kufasiriwa ili watu waelewe maana ya ujumbe unaowasilishwa.

Kwa upande mwingine, kuna tahadhari nyingine zinazopitishwa kwa njia maneno pekee ila michoro au ishara.Tahadhari kama hizi zimetamalaki katika pakiti za bidhaa tunazotumia manyumbani mwetu au pakiti za dawa kwa mfano.

Tahadhari huweza kuwekwa mahala maalumu ambapo tahadhari inahitajika na ambapo zitaonekana kwa urahisi. Mathalani tahadhari nyingi za barabarani huweza kuwekwa pahala palipo wazi na ambapo tahadhari hiyo inahitajika zaidi.Iwapo pana pahala penye mteremko,itawekwa kwani ndipo panafaa
Kwa upande mwingine, baadhi ya tahadhari huwekwa kwenye mavazi kama vile shati

**Matumizi ya Lugha katika tahadhari**

Lugha ya tahadhari ina sifa zifuatazo:-
Lugha ya tahadhari ni sahili
Lugha huwa rahisi kueleweka
Aghalabu maneno huandikwa kwa herufi kubwa na kwa wino mzito
Mara nyingi huandikwa kwa rangi nyekundu ili kutilia mkazo ujumbe unaowasilishswa.
Hutumia viakifishi kama vile alama hisi au kiulizi ili kuujaliza ujumbe.
Kutokana na mifano ya tahadhari uliyopewa, jibu maswali yafuatayo kwa kusema kama ni kweli au si kweli

**Lugha ya tahadhari ni sahihi (kweli / si kweli)**

Onyo / ilani huandikwa kwa herufi kubwa na wini mzito (kweli / si kweli)
Mara nyingi ilani haziambatani na mchoro (kweli / si kweli)
Ilani / onyo hazieleweki kwa urahisi (kweli / si kweli)
katika tahadhari za hatari, mchoro ya kuogofya hutumika (kweli / si kweli)

**Utangulizi**

Tazama picha ifuatayo na utaje inahusisha sherehe gani?

Je, Ratiba ni nini?
Ili kufanikisha sherehe kama hizo ni lazima kuwe na mpango maalumu ambao utafuatwa ndipo sherehe ziendeshwe vizuri.
Mpango huu huitwa RATIBA.Yaani utaratibu unaoonyesha matukio yanayotarajiwa kutendeka (hatua kwa hatua)

Hatua hizi hujikita kwa muda uliowekwa.
Shughuli fulani huchukua muda mahususi ambao huandikwa kwenye ratiba.
Kwa kifupi, ratiba huonyesha jambo litakalofanywa, nani atakayehusika na wakati wa kutekeleza.

Mahali pa sherehe: Kanisa la mtakatifu Francis wa Assisi, Mlaleoni
Ukumbi wa Rahatele, Mlaleoni 8.30 - 9.30 asubuhi: Bi Arusi achukuliwa nyumbani kwa wazazi wake
9.30 - 10.00 asubuhi: Safari kuelekea kanisani
10.00 - 10.30 asubuhi: Kufika kanisani na kujiandaa kwa ibaada
10.30 - 12.00 mchana: Ibaada ya Arusi
12.00 - 12.30 mchana: Kupiga picha
12.30 - 1.30 Mchana: kuelekea kwenye ukumbi.

1. -2.30 alasiri:Mlo na vinywaji
2. - 3.30 alasiri: Mawaidha:

3.30 - 4.30 jioni: Kutoa zawadi
4.30 - 5.00 jioni: Kukata keki
5.00 - 5.15 jioni: Kutoa shukrani

Ikumbukwe kuwa, uandishi wa ratiba hutegemea aina ya sherehe na muda uliotengwa.
Muda hurejelewa kwa kuzingatia utaratibu wa usomaji saa wa kimataifa.

**Umuhimu wa Ratiba**

Ratiba ni muhimu kwa sababu;
Hufahamisha shughuli za sherehe,
Hubainisha mfuatano wa shughuli,
Huonyesha mgawanyo wa muda,
Hufahamisha wanaopaswa kutenda majukumu fulani maalamu,
Huwawezesha wahusika kujiandaa ipasavyo,
Hujulisha, kwa ujumla, kiini cha sherehe,
Huhakikisha mtiririko mzuri wa shughuli na matumizi bora ya muda.